

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI**

Simu: +255 026 2322602
Tovuti: www.maji.go.tz
Barua pepe: ps@maji.go.tz



Mji wa Serikali,
Mtaa wa Maji,
P. O. Box 456,
DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MAADHIMISHO YA WIKI YA MAJI KITAIFA (WATER WEEK) MWAKA 2020

Mwezi Desemba 1992 Umoja wa Mataifa, kupitia Azimio Na. 47/193, ilitenga tarehe 22 Machi kuwa Siku ya Maji Duniani na ikaanza kuadhimishwa rasmi mwaka 1993. Siku hii hutumika kuhamasisha jamii kulinda na kuendeleza rasilimali za maji, na kuhimiza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wote.


Nchi yetu pia imekuwa ikiadhimisha Siku ya Maji kila mwaka kwa kuandaa Wiki ya Maji. Wiki ya Maji huambatana na matukio mbalimbali kulingana na Kauli Mbiu ya mwaka huo.

Mwaka huu Wiki ya Maji itaadhimishwa kuanzia tarehe 16 Machi hadi tarehe 22 Machi, 2020. Katika wiki hii, nchi yetu itaungana na mataifa mengine duniani katika kutathmini mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika sekta ya maji katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Maadhimisho haya yataambatana na matukio yafuatayo:

- (i) Uzinduzi wa miradi ya maji
- (ii) Mkutano wa Kisayansi wa Wataalamu wa Maji (Water Scientific Conference) utakaofanyika tarehe 17-18 Machi 2020 katika Ukumbi wa Mikutano wa Hoteli ya APC uliopo Mbweni Jijini Dar es Salaam. Mkutano huu utafunguliwa rasmi na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** tarehe 17 Machi, 2020. Kauli mbiu ya Mkutano huu, ambao ndiyo Kauli Mbiu ya Siku ya Maji Duniani, ni ***"Maji na Mabadiliko ya Tabia nchi: Uhakika wa Maji Salama kwa Wote (Water and Climate Change: Ensuring Water Security for All).***

- (iii) Mkutano wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira utakaofanyika tarehe 19-20 Machi, 2020. Lengo la mkutano huu ni kujadili mafanikio na changamoto za Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira katika kufikisha huduma ya maji kwa wananchi. Pamoja na mambo mengine, Mkutano huu utapokea taarifa ya utendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kutoka kwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Nishati na Maji (EWURA). Taarifa ya tathmini ya utendaji wa Mamlaka itazinduliwa na ***Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (MB), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.***
- (iv) Mkutano wa Pamoja kati ya Serikali na Wadau wa Sekta ya Maji (**Joint Water Sector Review**) utakaofanyika tarehe **21 Machi, 2020.** Mkutano huu utakutanisha Serikali na washirika wa maendeleo na wadau mbalimbali wanaochangia katika maendeleo ya sekta ya maji, na watajadili, pamoja na mambo mengine, vyanzo vya fedha kwa ajili ya sekta ya maji.

Kwa niaba ya Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa (MB), ninawakaribisha wananchi wote kushiriki katika kuadhimisha Wiki ya Maji. Wizara ya Maji inaamini na kutambua kuwa kila moja wetu ana nafasi na jukumu la kulinda, kutunza na kuendeleza raslimali za maji, na katika kuhakikisha kuwa huduma ya maji na usafi wa mazingira inawafikia wote.



Prof. Kitila Mkumbo

KATIBU MKUU

Dodoma

12 Machi 2020.